

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO

Telegram "AFYA", DODOMA  
Nambari ya Simu: +255 026 – 2323267  
E- Mail Na. [ps@afya.go.tz](mailto:ps@afya.go.tz)



Mji wa Serikali Mtumba,  
Barabara ya Afya,  
S.L. P 743,  
40478 DODOMA.

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

**TAARIFA YA MWENENDO WA UGONJWA WA CORONA (COVID-19) NCHINI**

**Dar es Salaam, Jumatano Aprili 08, 2020**

Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto inathibitisha kuwepo kwa mgonjwa mpya mmoja (01) mwenye maambukizi ya virusi vya corona (COVID- 19) jijini Dar es Salaam. Mgonjwa huyo ni mwanaume mwenye umri wa miaka (51) raia wa Tanzania, mkazi wa Dar es Salaam. Mgonjwa yuko chini ya uangalizi wa watoa huduma za afya katika kituo maalum cha tiba Dar es Salaam. Wizara ya Afya inaendelea kuwafuatilia watu wa karibu (contacts) waliowahi kukutana na mgonjwa huyu.

Hivyo, hadi sasa jumla ya watu ishirini na watano (25) wamethibitika kuwa na maambukizi ya COVID-19 tangu kuanza kwa ugonjwa huu nchini. Wagonjwa hawa ni pamoja na wale waliotolewa taarifa kutoka Zanzibar ambapo kati ya hawa wagonjwa watano (5) wamepona na mgonjwa mmoja (1) amefariki. Aidha, toka turipoti mgonjwa wa kwanza wa COVID-19 nchini hadi kufikia leo tarehe 8 Aprili, 2020 saa 5 asubuhi jumla ya watu 789 waliokutana na wagonjwa (contact) wanafuatiliwa kwa karibu. Aidha, kuanzia tarehe 24 Machi, 2020 hadi sasa jumla ya wasafiri 2,181 wamewekwa karantini nchini na kati ya hawa wasafiri 324 wamemaliza siku 14 za uangalizi.

Ili kuzuia kuenea kwa maambukizi ya COVID-19 katika jamii, Serikali inatoa msisitizo kwa wananchi kuzingatia maelekezo ya wataalam wa afya ya kujikinga na maambukizi ya virusi vya Corona (COVID- 19) hususan kwa kunawa mikono kwa sabuni na maji tiririka. Aidha, tunawasisitiza wananchi pia kuzingatia maelekezo mengine yanayohusu kuepuka mikusanyiko isiyo ya lazima na kukaa umbali usiopungua mita moja kati ya mtu na mtu.

Umyy A. Mwalimu (Mb)

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII,  
JINSIA, WAZEE NA WATOTO**

